



**JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA**

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

IDARA YA UKUZAJI VIUMBE MAJI

**UTARATIBU WA KUPATA KIBALI CHA
KUANZISHA UFUGAJI SAMAKI
KIBIASHARA**



TAARIFA MUHIMU

Ukuzaji viumbe maji wakibiashara unajumuisha ufugaji wowote wenye mtaji mkubwa au unaoweza kuwa na athari katika mazingira na jamii. Hii ni pamoja na ufugaji samaki katika vizimba ndani ya maziwa, mito na bahari. Kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 zinamtaka mwekezaji kupata kibali ili kufanya ufugaji huo. Kibali hicho hutolewa na Mkurugenzi wa Ukuzaji Viumbe Maji baada ya mwekezaji kujaza fomu Na. 7 (angalia mfano wake upande wa pili) ikiwa na viambatanisho vifuatavyo:

1. Uthibitisho wa kumiliki eneo la kukuzia viumbe maji husika. Uthibitisho huo unaweza kuwa ni hati ya kumiliki ardhi au muhtasari wa mkutano wa kijiji unaoonyesha wananchi wa eneo husika kuridhia kutoa ardhi kwa mwekezaji kuhusiana na ukuzaji viumbe maji (*Land Ownership/Title Deed*).

2. Ripoti ya Tathmini ya Athari ya Mazingira (*Environmental Impact Assessment Report*) kuhusu ufugaji unaotarajiwa kufanywa iliyothibitishwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC)

3. Kibali cha Matumizi ya Maji kutoka mamlaka ya usimamizi wa maji kwenye bonde husika (*Water User Right Permit*)

4. Ramani inayoonyesha mpangilio wa mabwawa, vizimba au matenki katika eneo la ufugaji (*Farm Layout*).

Ikiwa mwombaji ni kampuni au ni kikundi cha jamii, inatakiwa kuwasilisha nyaraka zote zinazothibitisha uhalali wa kampuni au usajili wa kikundi husika kwa mujibu wa sheria.

Fomu Na. 7 iliyojazwa kikamilifu ikiwa na viambatisho na barua ya maombi itumwe kwa:

Katibu Mkuu (Uvuvi),
Wizara ya Mifugo na Uvuvi,
S.L.P 2847,
40487 Dodoma
Simu: +255 26 2322612
Nukushi: +255 (0)2861908
E-mail: ps@uvuvi.go.tz

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia:

Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji,
Wizara ya Mifugo na Uvuvi,
S.L.P 2847,
40487 Dodoma
Simu: +255 (0)769220212
Nukushi: +255 (0)2861908
E-mail: daq@uvuvi.go.tz

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
THE FISHERIES ACT, 2003
(The Fisheries (Amendment) Regulations 2009)
(Regulation 31(1), 37(a))

Affix recent
coloured
passport size
photograph

APPLICATION FOR A PERMIT TO ESTABLISH A COMMERCIAL/LARGE SCALE AQUA FARM

PART ONE

1. Application is hereby made for the establishment of a commercial aqua farm for raising of(common/species name)
2. Applicant's particulars:
 - (a) Full name
 - (b) Occupation.....
 - (c) Postal address.....
 - (d) Telephone No.....Mobile phone.....E-mail.....
 - (e) Physical business address.....
 - (f) Residential address.....
 - (g) Nationality.....
 - (h) If Tanzania citizenship has been acquired by registration, state registration number.....
 - (i) For non Tanzanian should attach work permit and investment permit from relevant authorities.
3. Particulars of the farm to be established:
 - (a) Type of culture system.....
 - (b) Type of technology.....
 - (c) Size of the farm(s) (hectare) situated atVillage WardDistrictRegion
 - (d) Source of water.....
 - (e) Attach the following: (i) Land ownership/title deed (ii) Environmental Impact Assessment Report (iii) Farm Layout Plan (iv) Water user Right permit
4. I certify to the best of my knowledge that, the above particulars are true.
 Full name of applicantDesignation.....
 SignatureDate.....

PART TWO

(To be filled in by District Fisheries Officer)

Recommendation

Name..... Signature.....Date

.....
Official Stamp

PART THREE

For official use only

(Approval by Director)

- i. This application is Approved/Not Approved
- ii. Reasons for not approving.....

Name.....Signature.....Date.....

.....
Official stamp

* Delete whichever is not applicable